**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE**

**015/1** **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 1**

(For Both School and Private Candidates)

**Muda: Saa 3** **MAJIBU** **Mwaka: 2017**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C na D zenye jumla ya maswali matano.
2. Jibu maswali yote
3. Kila swali lina alama 20



Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

***Prepared by: Maria Marco for TETEA***

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha andika herufi yake katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Sunnah ni mwenendo wa mafundisho ya Mtume (s.a.w) wakati Hadithi ni
A matendo ya maswahaba wa Mtume (s.a.w)
B taarifa juu ya Sunnah
C mapokezi timilifu ya taarifa iliyotolewa na maswahaba
D matendo na taarifa za awali za Mtume (s.a.w)
E sehemu ya mafundisho ya Qur'an.
Jibu: D
Sababu: Sunnah inahusiana na mwenendo na mafundisho ya Mtume (s.a.w), wakati Hadithi ni mapokezi ya taarifa kuhusu Sunnah yake.

(ii) Sunnah ya Mtume (s.a.w) inafahamika mpaka hivi leo kwa sababu ipi?
A Mtume (s.a.w) tangu mwanzoni mwa utume aliwaamuru Waislamu waandike Sunnah yake.
B Yeye mwenyewe Mtume (s.a.w) alichukua dhima ya kuandika Sunnah yake.
C Maswahaba walimuiga Mtume (s.a.w) na kuhifadhi mafundisho yake katika vifu vyao na katika maandishi.
D Tabiina walitumia sana Hadithi za Mtume (s.a.w) kutoa fatwa zao.
E Waumini waliifanya Sunnah ya Mtume (s.a.w) ndiyo dira ya kuitafsiri Qur'an katika matendo.
Jibu: C
Sababu: Maswahaba walikuwa waangalifu sana katika kuhifadhi mafundisho ya Mtume kwa kuyahifadhi katika nyoyo na maandishi.

(iii) Mwandishi wa kitabu cha Hadithi cha Al-Qatadaya kilichoandikwa wakati wa maswahaba ni nani?
A Ibn Abbas (r.a).
B Abubakar (r.a).
C Ali bin Abu-Twalib (r.a).
D Ummar bin Khatab (r.a).
E Uthman bin Affan (r.a).
Jibu: A
Sababu: Ibn Abbas (r.a) alihifadhi na kuandika Hadithi za Mtume (s.a.w) na kitabu chake cha Al-Qatadaya kimekuwa maarufu katika historia.

(iv) Hadithi kamilifu imegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni
A Isnad na Matini
B Sahihi na Hassan
C Qudus na An-Nabawy
D Ahad na Mutawatir
E Maudhui na Hassan
Jibu: A
Sababu: Sehemu mbili kuu za Hadithi ni Isnad (msururu wa wapokezi) na Matini (maudhui ya maneno).

(v) "Rawahu As-habu Sunani" pia ina maana sawa na



Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

***Prepared by: Maria Marco for TETEA***

A Rawahu Muslim
B Rawahu Khamsa
C Rawahu Abu Daud
D Rawahu Arbaa
E Rawahu Bukhari
Jibu: D
Sababu: “Rawahu As-habu Sunani” inahusiana na masahaba wanne wa vitabu vya Sunan.

(vi) Ni tukio lipi lililotokea katika kipindi cha maswahaba na kuufanya uandishi wa Hadithi za Mtume (s.a.w) kuwa muhimu?
A Kutoweka kwa maswahaba wa Mtume (s.a.w).
B Mgogoro wa kumpata Khalifa wa kwanza (s.a.w).
C Kuzuka kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe miongoni mwa maswahaba.
D Kuzuka kwa Hadithi za uongo.
E Kupanuka kwa dola ya Kiislamu.
Jibu: D
Sababu: Kuzuka kwa Hadithi za uongo kulifanya iwe muhimu kuanza kuchuja na kuandika Hadithi sahihi.

(vii) Matini ya Hadithi za Mtume (s.a.w) maana yake ni
A mapokezi ya Hadithi zaidi ya moja
B ufafanuzi wa Qur’an tukufu
C kigezo cha usahihi wa Isnad
D kauli au matendo ya Mtume (s.a.w)
E kauli na matendo ya Muhadithina.
Jibu: D
Sababu: Matini ni maudhui halisi ya maneno au matendo yaliyopokelewa kutoka kwa Mtume (s.a.w).

(viii) Katika kipindi cha Maswahaba (Tabii-Tabiina), wanazuoni waliofanya elimu ya Hadithi kuwa fani miongoni mwa fani za elimu ya Kiislamu ni
A Suyut na Ibn Hajar Asqalaha
B Bukhar na Muslim
C Ahmad bin Hambal na Malik bin Anas
D Umar bin Abdul-Aziz na Suyut
E Tabaran na Al-Qutmy
Jibu: C
Sababu: Ahmad bin Hambal na Malik bin Anas walichangia kuifanya elimu ya Hadithi kuwa fani ya kitaalamu ya Kiislamu.

(ix) Katika mwaka wa 11 hadi 101 AH matatizo mengi yalitatuliwa kwa hukumu zilizotokana na
A maamuzi ya shura
B sharia za Kiislamu
C watalalamu wa Bani Umayah
D sharia za mahakama zilizotungwa na maswahaba


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

***Prepared by: Maria Marco for TETEA***

E Hadithi zilzohifadhiwa na maswahaba
Jibu: E
Sababu: Katika kipindi hiki, maswahaba walihifadhi Hadithi na kuzitumia kutatua masuala ya jamii Kiislamu.

(x) Miongoni mwa mambo muhimu ambayo yanatia nguvu usahihi wa Hadithi ni
A ushiriki wa mpokezi wa jihadi
B umri wa mpokezi
C uzalendo wa mpokezi
D imani ya mpokezi
E udhibitifu wa mpokezi.
Jibu: E
Sababu: Udhibitifu wa mpokezi ni muhimu kwa sababu unathibitisha uaminifu na usahihi wa taarifa zinazotolewa na mpokezi.

2. Oanisha maudhui ya Qur’an yaliyopo katika Orodha A na Sura za Qur’an zilizopo katika Orodha B. Andika herufi ya jibu sahihi kutoka Orodha B pembeni ya namba kutoka Orodha A katika kijitabu chako cha kujibia.

Orodha A
(i) Sura nzima ya mwisho kushushwa kwa Mtume (s.a.w).
(ii) Aya tano zilizoifuatania zikihimiza wanadamu juu ya swala la kujielimisha.
(iii) Allah (s.w) alionesha kuwepo kwake na uwezo wake pale alipomthilikisha Abraha na jeshi lake.
(iv) Qur’an ilianza kushushwa katika usiku wenye cheo.
(v) Sura ndefu kuliko sura zote katika Qur’an.
(vi) Ili mwanadamu apate kufuzu hapa duniani na Akhera hana budi kuchunga muda.
(vii) Sura inayojulikana kwa jina la Ummul-Kitaab.
(viii) Mwanadamu ameghafilika na neema za hadhi yake hapa ulimwenguni na kupupia wingi wa mali, wake na watoto.
(ix) Qur’an ilishushwa kwa lengo la kuwaongoza wanadamu.
(x) Tutakosomeshwa (tutakosomwa) wala hutasaaha. Ila akipenda Mwenyezi Mungu.
(xi) Tumtume Allah (s.w) mahitaji yetu mbalimbali kwa kutanguliza sifa zake tukufu.
(xii) Al-Muawidhatani ni jina la pamoja la Sura mbili.
(xiii) Makuraysh walimkata Mtume (s.a.w) ashirikiane nao katika ibada.
(xiv) Ardhi itatoa maelezo ya mambo yote yaliyotokea duniani.
(xv) Miongoni mwa miujiza ya Qur’an ni kutosilimu kwa ami yake Mtume (s.a.w) mpaka kufa kwake.

Orodha B
A Al-Alaq
B Al-Fatihah
C Al-Baqara
D Az-Zil-Zal
E Al-Lahab


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

***Prepared by: Maria Marco for TETEA***

F Al-Kauthar
G Al-Imran
H Al-Qadr
I Al-Asr
J Al-Alaa: 6-7
K Al-Muawidhatani
L Al-Fatihah: 2-5
M Quraish
N An-Nasr
O Al-Fil
P Al-Asr
Q Al-Fil

Majibu:
(i) N
(ii) A
(iii) O
(iv) H
(v) C
(vi) I
(vii) B
(viii) F
(ix) G
(x) J
(xi) L
(xii) K
(xiii) M
(xiv) D
(xv) E

3. Panga vipengele vya (a), (b) na (c) katika mtiririko wenye kuleta mantiki. Andika herufi na namba tu zinazohusika katika Kijitabu chako cha Kujibia.

(a) Katika Uislamu hakuna imani ya kibubusa.
(i) Aliyemuumba awali atashindwaaje kumba mara ya pili?
(ii) Miongoni mwa hoja kubwa za wakanaao ufufuo ni kuwa ni muhali mtu kufufuka baada ya kuoza na mifupa yake kusagikasagika.
(iii) Ulimbe la mbingu na ardhi, nafsi ya mwanadamu na historia ya Mitume ni miongoni mwa alama kuu za kuthibitisha kuwa Allah (s.w).
(iv) Pamoja na miujiza waliyopewa mitume kuna alama nyingine mbalimbali zinazothibitisha kuwepo kwa Allah (s.w).
(v) Kumkansha Allah (s.w) kunakwendana sambamba na kukanausha kuwepo siku ya malipo.
Jibu: (iii), (iv), (ii), (i), (v).

(b) Ili mwanadamu aepukane na kiburi kutokana na fadhila alizopewa ni muhimu azingatie maneno ya Allah (s.w) yafuatayo:
(i) Bila shaka wewe ni mwenye uwezo juu ya kila kitu.
(ii) Kheri imo mikononi mwako.
(iii) Sema, ewe Mola uliyeimiliki ulimwengu wote.
(iv) Na humtukuza umtakaye na humdhalilisha umtakaye.
(v) Humpa ufalme umtakaye na humvua uongozi umtakaye (3:26).
Jibu: (v), (iii), (ii), (i), (iv).

(c) Roho ya mwanadamu ni ya milele inakuepo katika vituo tofauti tofauti tangu kuumbwa kwake.
(i) Kuumbwa kwa roho mbalimbali na kuhurudishwa mbele ya Allah (s.w).
(ii) Roho kuadhibiwa au kustareheishwa.
(iii) Roho kuitwa katika mimba ya mama.
(iv) Kukiri kwa roho hizo mbele ya Allah (s.w) kuwa ndiye muumba wao.
(v) Roho kujitenga na mwili.
Jibu: (i), (iv), (iii), (v), (ii).

4. Jibu maswali yafuatayo kwa kifupi kwa kuandika majibu katika kijitabu chako cha kujibia.

(a) Ili kuthibitisha kuingia katika Uislamu mtu hutakiwa kufanya jambo gani? Taja jambo hilo.
Jibu: Kusoma shahada kwa dhati na kukubali kwamba hakuna Mungu isipokuwa Allah na Muhammad ni Mtume wake.

(b) Nguzo za tayammam ni nne; taja nguzo mbili tu kati ya hizo.
Jibu:
i. Nia ya kufanya tayammam.
ii. Kupangusa uso na mikono kwa mchanga safi.

(c) Orodhesha swala ambazo haziingii katika tahfifu ya kupunguza rakaa.
Jibu:
i. Swala ya Alfajiri.
ii. Swala ya Magharibi.

(d) Taja mambo mawili ambayo yakifanywa ibada ya Umra hukamilika.
Jibu:
i. Kutufu Kaaba mara saba.
ii. Kukata nywele au kunyoa kichwa.

(e) Bainisha nisaab ya ng’ombe na kiasi cha kutoa.
Jibu:
i. Nisaab ya ng’ombe ni 30.
ii. Kiasi cha kutoa ni ndama mmoja wa mwaka mmoja kwa kila ng’ombe 30.

(f) Ainisha sifa mbili za mashahidi wanaopaswa kushuhudia ndoa ya Kiislamu.
Jibu:
i. Mashahidi wawe Waislamu wenye akili timamu.
ii. Mashahidi wawe waadilifu na waaminifu.

(g) Orodhesha mambo mawili yanayoharibu funga (swaumu) ya mtu.
Jibu:
i. Kula au kunywa kwa makusudi wakati wa funga.
ii. Kujamiiana mchana wa mwezi wa Ramadhani.

(h) Tofautisha kati ya mfumo wa uchumi wa Kiislamu na wa Kijahilini kuhusu dhana ya bidhaa.
Jibu:
i. Uchumi wa Kiislamu unasisitiza biashara halali na haki.
ii. Uchumi wa Kijahilini ulisisitiza riba na unyang'anyi.

(i) Elezea tofauti iliyopo kati ya adhabu ya mlevi na ya mzinifu.
Jibu:
i. Mlevi huadhibiwa viboko 40 au zaidi kwa mujibu wa sheria.
ii. Mzinifu aliyefunga ndoa huadhibiwa kwa kupigwa mawe hadi kufa, na ambaye hajafunga ndoa viboko 100.

(j) Toa maelezo mafupi kuonyesha jinsi msafiri alivyorahisishiwa swala.
Jibu:
i. Kupunguza swala za rakaa nne hadi rakaa mbili.
ii. Kuruhusiwa kuunganisha swala mbili kama Dhuhur na Asr au Magharibi na Isha.

(k) Taja sifa mbili za Waislamu wanaolazimika kufunga mwezi wa Ramadhani.
Jibu:
i. Kuwa Muislamu mwenye akili timamu.
ii. Kuwa na uwezo wa kimwili wa kufunga.

(l) Orodhesha mambo mawili yanayomzuia mtu kurithi mali.
Jibu:
i. Kuua anayempa urithi.
ii. Kuasi dini ya Kiislamu.

(m) Bainisha hukumu ya mwanamke aliyeachwa na mume mara baada ya kufunga ndoa lakini hawajafanya tendo la ndoa.
Jibu: Mwanamke ana haki ya nusu ya mahari aliyoahidiwa.

(n) Andika tafsiri ya aya inayonyesha lengo la kutoa zaka.
Jibu: "Chukua sadaka katika mali zao ili uwasafishe na kuwatahirisha kwa hizo, na uwaombee; hakika du'a yako ni utulivu kwao." (9:103).

(o) Bainisha nafasi ya Mwenyezi Mungu na mwanadamu katika falsafa ya umiliki mali kwa mtazamo wa Uislamu.
Jibu:
i. Mwenyezi Mungu ndiye mmiliki wa mali zote.
ii. Mwanadamu ni msimamizi na mlinzi wa mali kwa niaba ya Mwenyezi Mungu.

5. Chagua neno au kifungu cha maneno (i) – (xxx) ili ukamilishe sentensi (a) – (o) kwa kuandika majibu sahihi tu katika kijitabu chako cha kujibia. Maneno au vifungu vya maneno vinaweza kutumika zaidi ya mara moja.

(a) Mambo mawili maarufu yanayoonyesha kuwa Mitume hawakuhathiriwi na mazingira katika maisha yao kabla ya kupewa utume kwa Mtume (s.a.w) ni ________ na ________.
Jibu: Mkweli, Mwaminifu.

(b) Makafiri wa Makka walimpinga Mtume (s.a.w) na utume wake kwa sababu za ________ na ________.
Jibu: Kudharauliwa, Ujinga.

(c) Wapinzani wa dola ya Kiislamu walikuwa Makafiri wa Kikureish na wasaidizi wao, ________, ________, na ________.
Jibu: Wayahudi, Wakristo, Munafiki.

(d) Serikali huwa ya Kiislamu pale inaendeshwa kwa misingi ya ________ na ________.
Jibu: Qur'an, Sunnah.

(e) Kwa mtazamo wa Uislamu, asili ya mwanadamu si ________; wala hadhi yake hapa ulimwenguni si sawa na ile ya mnyama kwani Qur’an inatufundisha kuwa binadamu wote ni watoto wa ________.
Jibu: Maovu, Adam na Hawa.

(f) Bilal alikuwa ________ na mtumwa wa ________ ambaye alikuwa adui mkubwa wa Uislamu.
Jibu: Mwaminifu, Umayya bin Khalaf.

(g) Miezi miwili baada ya ________, Mtume (s.a.w) alishikwa na ________.
Jibu: Aqaba, Hijjatul-wadai.

(h) Kikundi cha Waislamu kiitwacho Khawarij walikubali mamlaka au ukhalifa wa ________ tu hawakumkubali ________.
Jibu: Qur'an, Abubakar na Omar.

(i) Miongoni mwa mateso ya kisaikolojia aliyoyapata Nabii Nuhu (a.s) kutoka kwa wapinzani wa ujumbe wa Mwenyezi Mungu ni ________ na ________.
Jibu: Kudhihakiwa, Kukataliwa.


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

***Prepared by: Maria Marco for TETEA***

(j) Wake wa Mtume Ibrahim (a.s) walikuwa ni mama ________ na ________.
Jibu: Hajir, Sarah.

(k) Mzigo mzito uliomvunja Mtume (s.a.w) unaotajwa katika sura ________ ni ________ yaliyodumu kwa muda mrefu.
Jibu: Al-Inshirah, Maovu.

(l) Kiongozi wa Hijra ya mwanzo kuelekea ________ alikuwa ni ________.
Jibu: Habasha, Jaffar bin Abuu Talib.

(m) Mikataba ya ________ ilisaidia sana katika kumhakikishia Mtume (s.a.w) kupata ________ kule Madina.
Jibu: Aqaba, Umma.

(n) Waislamu wa Tanganyika walikuwa mstari wa mbele katika ________ kutokana na kunyanyaswa kwao ________.
Jibu: Kupigania uhuru, Kiuchumi.

(o) Kutokana na utukufu wake mji wa Makka pia umeitwa katika Qur'an kwa jina la ________ yaani mama wa mji (Qur'an 42:7) na pia umeitwa ________ yaani mji wa amani (Qur'an 95:3).
Jibu: Ummul-Qura, Al-balad-amin.


Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

***Prepared by: Maria Marco for TETEA***